

Ushauri wa Jinsi ya Kutumia Hundi za Matunda na Mboga (ukurasa wa 6)--angalia picha ya hundi iliyo hapa chini:

1. Hundi ya Matunda na Mboga inaweza kutumiwa katika duka lililoidhinishwa na WIC, Soko la Wakulima au Kibanda cha Kuuzia Mazao.

② Angalia tarehe kwenye hundi ya WIC. Tarehe ya kwanza ni siku ya kwanza ambayo unaweza kutumia hundi. Tarehe ya pili ni siku ya mwisho ambayo unaweza kutumia hundi. Unaweza kutumia idadi yoyote ya hundi za WIC ambazo zinatumiwa katikati ya tarehe hizi kwa wakati mmoja.

③ Angalia kiasi cha dola kilichoorodheshwa kwenye hundi yako ambacho WIC itagharimia.

4. Weka matunda yote na mboga kwa vikundi utakapokuwa kwenye sehemu ya kulipia bidhaa.

5 Mpe keshia folda yako ya WIC na hundi ambazo unatumia kabla ya bidhaa za chakula za WIC kupitishwa kwenye kitambazo cha msimbo pau.

⑥ Andika jumla ya bei ya bidhaa za chakula za WIC kwenye hundi isipokuwainachapopishwa kiotomatiki na sajili ya pesa ya duka. Kiasi cha pesa kilichoandikwa hakiwezi kuzidi thamani ya hundi. Ikiwa jumla ya kiasi cha pesa kinazidi thamani ya hundi ya matunda na mboga, ni lazima ulipe kiasi kilichozidi. Kwa mfano:

- Thamani ya Hundi ya Matunda na Mboga ni \$11.00.
- Bidhaa ulizonunua zimegharimu jumla ya \$12.00.
- Ni lazima ulipe kiasi cha \$1.00 kilichozidi.

Ikiwa jumla ya bei za matunda na mboga ulizonunua ni ndogo kuliko thamani ya hundi, hautarudishiwa pesa zozote.

⑦ Tia sahihi kwenye upande wa mbele wa hundi katika sehemu ya chini kulia na kisha umrejeshee keshia hundi hiyo. Keshia atahakikisha sahihi yako inasawiana na sahihi ya mwakilishi aliyeidhinishwa, mshiriki au wakala aliye kwenye Folda ya WIC.

8. Hakikisha umerejeshewa folda yako na risiti kabla ya kuondoka kutoka kwenye sehemu ya kulipia bidhaa, Soko la Wakulima au Kibanda cha Kuuzia Mazao.

MAINE WIC NUTRITION PROGRAM Department of Health and Human Services
 11 SHS, Augusta, Maine 04333 - 1-800-437-9300 - www.WICforME.com

NAME OF PARTICIPANT		FIRST DAY TO USE	LAST DAY TO USE	CHECK NUMBER
SAMPLE CHECK		3/23/2016	4/22/2016	03356297
PARTICIPANT I.D.	AGENCY	CLINIC	FOOD PACKAGE	FI TYPE
10043571				
FOR PURCHASE OF APPROVED WIC FOODS ONLY (NO SUBSTITUTIONS ALLOWED):			AMOUNT	STAMP BELOW
\$11.00 For Fresh, Frozen or Canned Fruits &/or Vegetables XXX END OF ORDER XXX			\$	
			DEPOSIT WITHIN 60 DAYS OF FIRST DAY TO USE PAY TO THE ORDER OF MAINE WIC VENDOR	
			X	
			SIGNATURE OF AUTHORIZED REPRESENTATIVE OR PROXY	